# Environmental Management and Biodiversity Conservation of Forests, Woodlands, and Wetlands of the Rufiji Delta and Floodplain

## Ripoti Ya Warsha Ya Uandaaji, Utekelezaji, Na Mapitio ya Sera na Sheria za Mazingira na Uzoefu wa Utekelezaji Katika Ngazi ya Wilaya na Vijiji na Zinavyoathiri Hali Halisi ya Maliasili Wilayani Rufiji Iliyofanyika Utete Rufiji Tarehe 3-5 Mei 2000

**(Proceedings of the seminar on 'the formualtion, implementaion, and review of environmental policies and legislation and their practice at District and Village levels: Their impacts on the natural resources status in Rufiji District' held in Utete, Rufiji, 3-5 May 2000.)**

**Imetayirishwa na Karanja, F[2], Hogan, R[3] & A, Shah[4]**



**Technical Report 8**

**July 2000**

**Mradi Usimamizi wa Mazingira Rufiji Utete, Pwani**
Project Manager,
Rufiji Environment Management Project
P O Box 13513
Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: 44 Utete Rufiji or 2666088 / 0741 322366 Dar es Salaam
Email: rempute1@bushmail.net or iucndar@epiq.or.tz

---

[1] The Rufiji District Council implements Rufiji Environment Management Project with technical assistance from IUCN – The World Conservation Union, and funding from the Royal Netherlands Embassy.
[2] Programme Officer (Natural Resources), IUCN EARO
[3] Technical Advisor-Community Development, REMP
[4] Project Manager, REMP

# Rufiji Environment Management Project - REMP

**Project Goal**
To promote the long-term conservation through 'wise use' of the lower Rufiji forests, woodlands and wetlands, such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area's inhabitants are secured and enhanced**.**

**Objectives**

- To promote the integration of environmental conservation and sustainable development through environmental planning within the Rufiji Delta and Floodplain.

- To promote the sustainable use of natural resources and enhance the livelihoods of local communities by implementing sustainable pilot development activities based on wise use principles.

- To promote awareness of the values of forests, woodlands and wetlands and the importance of wise use at village, district, regional and central government levels, and to influence national policies on natural resource management.

## Project Area

The project area is within Rufiji District in the ecosystems affected by the flooding of the river (floodplain and delta), downstream of the Selous Game Reserve and also including several upland forests of special importance.

**Project Implementation**
The project is run from the district Headquarters in Utete by the Rufiji District Administration through a district Environmental Management Team coordinated by the District Executive Director. The Project Manager is employed by the project and two Technical Advisers are employed by IUCN.
Project partners, particularly NEMC, the Coast Region, RUBADA, The Royal Netherlands Embassy and the Ministry of Natural Resources and Tourism, collaborate formally through their participation in the Project Steering Committee and also informally.

**Project Outputs**
At the end of the first five –year phase (1998-2003) of the project the expected outputs are:
An Environmental Management Plan: an integrated plan for the management of the ecosystems (forests, woodlands and wetlands) and natural resources of the project area that has been tested and revised so that it can be assured of success - especially through development hand-in-hand with the District council and the people of Rufiji.

Village (or community) Natural Resource Management Plans: These will be produced in pilot villages to facilitate village planning for natural resource management. The project will support the implementation of these plans by researching the legislation, providing training and some support for zoning, mapping and gazettement of reserves.

Established Wise Use Activities: These will consist of the successful sustainable development activities that are being tried and tested with pilot village and communities and are shown to be sustainable

Key forests will be conserved: Forests in Rufiji District that have shown high levels of plant biodiversity, endemism or other valuable biodiversity characteristics will be conserved by gazettement, forest management for conservation, and /or awareness-raising with their traditional owners.

# Table of Contents


**1 Utangulizi** ..... **1**

1.1 Malengo ya Semina ..... 1
1.2 Shukrani ..... 3

**2 Ufunguzi wa Seminar** ..... **4**

2.1 Hotuba tz Kufungua Semina ..... 4

**3 Mada Zilizoongelewa (MEI 3-4, 2000)** ..... **5**

3.1 Mada Kuhusu Sera na Sheria za Mazingera ..... 5
3.2 Majadiliano juu ya Mada Zilizotolewa ..... 5
3.3 Majadiliano ya Vikundi Kuhusu Sera na Sheria ..... 7

**4 Mada zilizoongelewa (Mei 5, 2000)** ..... **10**

4.1 Hali ya sasa ya Uangushaji Na Uvunaji Misitu Wilayani Rufiji ..... 10
4.2 Rasilimali ya Miti ya Mbao Katika Wilaya ya Rufiji ..... 10
4.3 Uhifadhi wa Mimea Mbalimbali Katika Wilaya ya Rufiji ..... 10
4.4 Uhifadhi wa Wanyama wa Aina Mbalimbali ..... 10
4.5 Maoni ya Wanasemina ..... 11

**5 Maoni ya Jumla** ..... **12**

**6 Kufunga Semina** ..... **12**

6.1 Hotuba ya Kufunga Warsha ..... 12

**7 Appendices** ..... **14**

# 1 Utangulizi

Moja ya malengo makuu ya awamu ya kwanza ya mradi ni kuboresha/kutambua thamani ya misitu, ardhi chepechepe na kufahamu umuhimu wa matumizi bora ya maliasili hizi katika ngazi za vijiji, wilaya, mkoa na serikali kuu na kuelekeza sera katika utunzaji wa maliasili.

MUMARU unalenga kuendeleza sera na sheria za mazingira katika Tanzania. Tunatambua umuhimu wa ILFEMP (NEMC na wizara ya Maliasili na Utalii na Wanachama) ambao kati ya mambo mengine inashauri kuundwa kwa Kamati za Mazingira za Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa na kuzipa nguvu Kata kuweka/kutunga sheria za kuboresha mazingira kati ya vijiji. Matatizo makubwa ambayo yapo katika sheria na sera zinazohusu mazingira ni kama:

Uhusiano mbovu kati ya serikali kuu na serikali za mitaa.
Udhaifu wa kuhakikisha kwamba sheria na sera zinatekelezwa ipasavyo
Elimu ndogo ya mazingira kwa waandaaji mipango na waamuzi wa utekelezaji
Mgongano kati ya wataalamu na wanasiasa
Udhaifu na upashanaji habari
Udhaifu wa wanasiasa kuelezea mambo ya mazingira
Uwezo mdogo wa watu na vitendea kazi vichache.

Kwa sasa hivi, sera na sheria nyingi zinazohusu mazingira zinapitiwa upya na zingine tayari zimekwisha tungwa upya. Kama sehemu ya mpango wa shughuli za mwaka 2000, pamoja na kuitikia wito wa ILFEMP na kutunga sheria na sera husika, MUMARU/REMP ilifanya semina/warsha ya siku moja juu ya sera na sheria mpya zinazohusu mazingira pamoja na kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira. Warsha/semina hii ilifanyika tarehe 3/4/200 hapa Utete, Rufiji. Washiriki walikuwa; Watumishi wa Wilaya, Madiwani, Viongozi ngazi za Kata na Vijiji pamoja na Wananchi wa kawaida toka katika vijiji vinne vya mfano na watumishi wa MUMARU.

Kwa ujumla, watu wa kawaida pamoja na viongozi hawapti habari na elimu juu ya sera na sheria mbalimbali. Kufahamu au kupata elimu ya sera na sheria ni muhimu sana kwani zinalenga katika uhifadhi mzuri wa maliasili. Katika ngazi ya wilaya, ingawa watumisni wanazijua sera na sheria, mara nyingi hawazifikishi kwa wananchi na washika dau wengine. Kama nyongeza, iwapo hizi sera na sheria zitatekelezwa ipasavyo, zitachangia katika uhifadhi na utunzaji mzuri wa maliasili za wilaya ya Rufiji, lakini, utekelezaji na ufuatiliaji wake umekuwa dhaifu sana kwa sababu mbalimbali , na mara nyingine zinapuuzwa tu. Ni kutokana na sababu hizi MUMARU iliamua kufanya semina ya siku tatu (3) ikiwa na lengo la kuwaelimisha washika dau juu ya hali halisi ya sera na sheria za mazingiara, kuangalia kwa kiwango gani sera na sheria hizi hufuatwa hapa wilayani na mwisho baada ya kufahamishwa juu ya sera na sheria zilizopo na upungufu uliopo katika utekelezaji, washika dau watachukua hatua kuhakikisha kwamba sera na sheria vinatekelezwa/vinafuatwa na kuchangia katika utunzaji mzuri wa maliasili ndani ya wilaya. Ni lengo la MUMARU kusambaza ujumbe huu kwa washika dau wote hapa wilayani ili uwe changamoto.

## 1.1 Malengo ya Semina

Semina iligawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza (May 3-5) ilizungumzia juu ya sera na Sheria za Mazingira na Ardhi. Watoa mada walikuwa wametoka Idara za serikali, Baraza la Utunzaji Mazingira (NEMC); Idara ya Misitu na Nyuki, na Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi (Nationa Land Use Planning Commission). Wakati wa semina watoa mada walisaidia kufanikisha mjadala juu ya;

Walipitia na kuchambua sera na sheria zilizopo za mazingira pamoja na sheria mpya za ardhi.
Kila mmoja alielezea hali halisi ya sasa na marekebisho yanayofanywa na wanasemina
Walijadili 1 na 2 hapo juu jinsi gani vinalingana na mipango ya kuhifadhi mazingira ya wilaya na vijiji vya mfano.

Watoa mada katika sehemu hii ya kwanza walikuwa;

- Mr. B. Kessy –(Kutoka Idara ya Misitu ya Nyuki) alitoa mada juu ya sera na sheria za misitu, Nyuki, wanyama pori na uvuvi

- Mr. Mwaipopo- (Kutoka Baraza la Kusimamia Mazingira-NEMC) alitoa mada juu ya sera na sheria juu ya mazingira, maji na maeneo chepechepe.

- Mr. Albert Mkama-(Kutoka Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi) alitoa mada ya sera na sheria zinazohusu Ardhi, Kilimo na Mifugo.

Sehemu ya pili ya semina (May 5) ililenga katika kuelezea hali halisi ya sasa ya maliasili za wilaya ya Rufiji. Watoa mada walilenga katika utafiti wa aina 4 ambao ulifanywa wilayani Rufiji kipindi cha February/March 2000. Hivyo warsha/semina hii ilitumika kama sehemu nzuri ya kuwaelezea washika dau matokeo ya watafiti.

Utafiti uliofanywa ulihusu

1. Kuelezea mimea iliyopo katika misitu iliyochaguliwa kwenye misitu ya Tambarare. Utafiti huu ulifanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Mimea (Botany Department). Malengo ya utafiti huu yalikuwa:

- Kuelezea mimea iliyopo kwenye misitu ya Tambarare
- Kuelezea maeneo nyeti yenye Bioanuwai nyingi na muhimu
- Kutafiti mimea ambayo itasaidia kuashiria hali ya mazingira
- Kupanga mpango wa muda mrefu wa kufuatilia aina hizi za mimea
- Mada hii ilitolewa na Mr. Mwasumbi toka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

2. Kutafiti aina kuu za jamii za wanyama wadogowadogo katika ukanda wa Tambarare ya mafuriko ya mto Rufiji. Kazi hii ilifanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam-Kitivo cha Zoologia.

- Malengo ya utafiti yalikuwa:
- Kutambua aina za wanyama wanyonyeshao, mijusi, vyura, ndege, kasa na viumbe vingineo
- Kutambua sehemu ambazo zina wanyama wengi wa aina hii
- Kutambua na kuelezea wanyama ambao watasaidia kuashilia hali halisi ya mazingira
- Kupanga mpango wa muda marefu wa kufuatilia maendeleo ya wanyama hawa.

3. Mada ya utafiti huu ilitolewa na Ndugu Kihaule toka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Tathmini ya aina kuu za miti ya mbao kwenye misitu ya miombo na ya kando kando mwa mito wilayani Rufiji. Utafiti huu ulifanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

- Malengo ya tathimini hii ni;
- Kujua kiasi cha miti ya mbao inayotumika wilayani
- Kukadiria uzalishaji endelevu wa miti hii ya mbao
- Mada ya utafiti huu ilitolewa na Mr. Stephano toka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine.

4. Kutathimini hali halisi ya uvunaji miti wilayani Rufiji. Kazi hii ilifanywa na Mr. Alistair Graham, A. Shah na R. Olivier.

Tathimini hii ilifanywa kwa kutumia ndege, na uhakika wa tathimini, ardhini umepangwa kufanyika miezi ijayo. Mada ya tathimini hii ilitolewa na Mr. Shah-Meneja wa Mradi wa MUMARU.

Maelezo haya yanafupisha warsha iliyofanyika kwa siku 3. Makabrasha kamili ya mada tatu juu ya sera na sheria za mazingira yameambatanishwa nyuma ya ripoti hii. Mada zingine nne juu ya hali halisi ya maliasili zinaendelea kutafsiriwa, zitatawanywa siku chache zijazo.

Ni tegemeo letu kwamba maelezo haya yatakuwa ni yenye maana nzuri na yenye msaada kwako, kwa kuwa moja ya kazi za MUMARU ni kutoa elimu juu ya mazingira. Tunakuomba ujumbe huu uwafikishie pia watu wengine kijiji kwako, Kata au Tarafa kwa kadri uwezavyo. Iwapo una matatizo

yoyote au unahitaji maelezo zaidi juu ya maswala au mambo yanayohusu sera na sheria za mazingira, unakaribishwa sana katika ofisi zetu hapa Utete.

## 1.2 Shukrani

Warsha hii isingeweza kuwa ni ya mafanikio mazuri bila nia njema na misaada toka kwa watu na Idara mbalimbali. Watoa mada Mr. Kessy, Mr. Mwaipopo, Mr. Mkama, Mr. Mwasumbi, Mr. Stephano, Mr. Kihaule na Mr. Shah, walitumia muda wao mwingi kutayarisha mada hizi.

Tunawashukuru sana kwa mchango wao binafsi wa kuendesha warsha hii kwa uadilifu mkubwa. Mr. Peter (DALDO-Rufiji), Mr. Nindai (DNRO-Rufiji) na Mr. Mwakalinga (Kilimo) walifanikisha kazi hii ya semina kwa kiwango cha juu. Sekretarieti pia ilifanya kazi nzuri ya kunukuu mambo muhimu yaliyoongelewa kwenye warsha hii, nayo ilikuwa ni; Ndugu, Peter (DALDO), Mr. Chilwa (Uvuvi), Mr. John (Wanyamapori) na Mr. Kinana Mussa (Afisa Misitu).

Mwisho, shukurani ziwaendee washiriki wote wa warsha kwa uzalendo na uchangamfu wao ambavyo vyote kwa pamoja vilikuwa ni vya kiwango cha juu.

---

**ASANTE SANA.**

# 2 Ufunguzi wa Seminar

Wanasemina walianza kuingia ukumbi wa semina saa 2.00 asubuhi na kujiandikisha. Kisha washiriki walijitambulisha mmoja mmoja kwa majina na kuelezea matarajio wanayoyategemea kutokana na semina hii. Karibu wanasemina wote walisema semina hii ni muhimu na wanatarajia kupata elimu ambayo itawasaidia katika kuhifadhi mazingira.

## 2.1 Hotuba tz Kufungua Semina

Iiliyotolewa na Ndugu F. Q. M. Fissoo, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Rufiji

Hatimaye mgeni rasmi Ndugu F.Q.M. Fissoo (Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Rufiji) alifungua rasmi semina hii. Katika ufunguzi huo alijaribu kuelezea madhumuni ya mradi wa MUMARU ambayo ni:

i) Kusisitiza mipango bora ya maliasili na kuimarisha maisha ya watu wa maeneo hayo kwa kuwezesha miradi ya maendeleo kwa misingi ya matumizi ya busara ya maliasili.
ii) Kuweka uwiano mzuri kati ya hifadhi, mazingira na maendeleo ya watu kwa kufanya mipango bora ya mazingira kwenye bonde la mto Rufiji, tambarare ya mafuriko pamoja na delta.
iii) Kuongeza ufahamu wa umuhimu wa matumizi ya busara ya maliasili vijijini, wilayani, mkoani nai serikali kuu (Taifa).

Mgeni rasmi alielezea kwamba wilaya hii imebahatika kuwa na maliasili nyingi (misitu, maziwa, mabwawa, mito, bahari, ardhi nzuri, wanyamapori, madini, n.k) lakini inasikitisha kwamba wananchi wake ni masikini. Alisisitiza sana utumiaji mzuri wa maliasili zetu ili zisipotee, na kusikitishwa kwa matumizi mabaya ya maliasili hizi. Alisema sasa hivi maliasili zetu zimekumbwa na matatizo mengi. Sheria zipo lakini hazitekelezwi na hakuna anayechukua hatua.

### 2.1.1 Matatizo aliyoyaelezea mgeni rasmi ni

**Uharibifu wa maliasili zetu**

1. Misitu inakatwa kwa wingi (mininga, mikongo, mivule hivi sasa imeanza kuwa adimu)
2. Vyanzo vya maji vinaharibiwa
3. Uvuvi haramu bado upo. Wavuvi wanatumia nyavu zenye matunda madogo hivyo huvuna samaki wasiostahili kuliwa.

**Umaskini**

Kiwango cha umasikini kwa wananchi wa Rufiji ni kikubwa.

Alitoa wito kwamba matatizo yote haya ili kuyatatua yanahitaji kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa kuwa na matumizi endelevu.

Mwisho mgeni rasmi alitoa changamoto kwa wanasemina wajadili kwa undani jinsi ya kuhifadhi mazingira na kuondoa umaskini kwa kutumia rasilimali zilizopo wailayani. Maliasili zipo, sheria zipo na nguvu kazi ipo. Kwa nini tuwe masikini?

Meneja mradi (Nd. A. Shah) naye alipata fursa ya kutoa maelezo mafupi juu ya mradi wa MUMARU. Alisema kwamba sehemu kubwa ya utafiti imekamilika na sasa wako katika utekelezaji na hasa maandalizi ya kutengeneza mpango wa uhifadhi wa mazingira.

# 3 Mada Zilizoongelewa (MEI 3-4, 2000)

## 3.1 Mada Kuhusu Sera na Sheria za Mazingera

Mada kuu tatu kuhusu sera na sheria za mazingira zilitolewa na kuongelewa katika semina

1. Utekelezaji wa sera na sheria za maliasili (Misitu, nyuki, uvuvi na wanayamapori) –mtoa mada ni Ndugu B. Kessy- Afisa Misitu Mkuu Kitengo cha Misitu na Nyuki – Dar es Salaam.
2. Sera na sheria ya mazingira (eneo chepechepe na maji). Mtoa mada ni Ndugu D. Mwaipopo – toka Baraza la Kuhifadhi Mazingira (NEMC) –Dar es Salaam.
3. Sera na sheria za ardhi na kilimo- Mtoa mada alikuwa Ndugu A. Mkama toka Tume ya Ardhi na Mipango – Dar es Salaam.

Wanasemina wote walipewa nakala za kila mada zilizotolewa ili wazitumie hapo baadaye kila mtoa mada alipomaliza kuwasilisha mada yake.

## 3.2 Majadiliano juu ya Mada Zilizotolewa

Kipindi cha majadiliano na maswali kilifuatia. Washiriki walionyesha kupevuka kwao na kukereketwa na mada za semina hii. Mchango mkubwa ulitolewa na washiriki na mambo yaliongelewa kwa njia ya maswali na utoaji maoni/hoja. Yafuatayo yaliongelewa:-

1. **Wanasemina walielezea wasiwasi wao wa kuwaelezea wananchi kuzitumia sera na sheria ambazo hazijapitishwa na bunge.**

   Mtoa mada aliwaondoa wajumbe wasiwasi wao kwa kuwaeleza kwamba sera za misitu ziliidhinishwa rasmi na serikali tangu March 1998 hivyo unaweza kutumika bila wasiwasi. Upande wa sheria za misitu ni kwamba bado sheria zile zile za zamani ndizo zinazopaswa kutumiwa.

2. **Katika sera za misitu serikali kuu inahodhi maeneo ya misitu serikali inaona ugumu gani kuzikabidhi halmashauri za wilaya na serikali ijiondoe**

   Sera mpya inaelezea kwamba serikali kuu sasa hivi itajiondoa katika shughuli za uendeshaji. Halmashauri, vijiji na watu binafsi watakabidhiwa maliasili zao kama ilivyo kwenye sera.

3. **Kilimo cha mwani kinaweza kuwapatia wananchi maendeleo lakini watu wengi hawajui juu ya hiki kilimo. Wananchi wameelimishwaje juu ya hiki kilimo hasa eneo la delta.**

   Maeneo nje ya wilaya ya Rufiji kilimo cha mwani kinaendeshwa. Rufiji bado utafiti haujafanywa na unatarajiwa kufanywa utafiti huo.

4. **Je, tuna imani gani kwamba sera zinapotungwa wananchi wanashirikishwa?**

   Sera zinapotungwa huwashirikisha wananchi kwa kupitia wawakilishi wao (wabunge na madiwani), wakurugenzi, mkuu wa wilaya , wataalam n.k

5. **Walitaka kujua ni nani wasimamizi wa hizi sera. Wanakijiji wana wajibu gani katika ulinzi wa maliasili kama kuwakamata wahalifu?**

   - Kila mtu ni msimamizi wa sera (wananchi, NGO, watumishi wa serikali. Kila mtu ana majukumu yake ya kutekeleza katika sera).

   - Wanakijiji wanayohaki ya kulinda maliasili zao na kuwakamata wahalifu na kuwapeleka sehemu zinazohusika kisheria.

**6. Hapa Rufiji ni wanawake wanaofanya kazi kama kilimo. Wanawake huko vijijini hawaelewi kuwa hii wilaya ina mradi wa mazingira. Pia mradi wa nyuki haufahamiki. Kuna sehemu wanapopatikana nyuki kwa wingi, je mnaonaje mradi wa nyuki ukianzishwa maeneo hayo?**

- Vijii vinavyofanyiwa kazi na mradi ni vya mfano tu sio vijiji vyote. Akina mama wote katika vijiji vya majaribio wanaufahamu huu mradi.

- Katika kamati za mazingira Idadi ya wajumbe akina mama ni sawa na ya akina baba au huweza kuzidiana kwa kiasi kidogo tu.

- Sasa hivi mtaalamu wa nyuki wa wilaya nzima yupo, hivyo kama mnamhitaji atakuja kutoa huduma.

**7. Wajumbe walitaka kujua wanashirikishwaje katika mradi wa ufugaji nyuki**

- Miradi ya nyuki ni kwa ajili ya watu wote wa jinsia zote na umri wa ngazi zote.

- Sera za mazingira zinahusu watu wote, wanawake wakiwemo.

**8. Bonde la mto Rufiji halina utafiti wa kutosha kiikolojia, kiuchumi n.k. Je, ni nani anastahili kufanya hivyo?**

- Taasisi mbalimbali zinazotumia bonde la mto Rufiji ndizo zinastahili kufanya utafiti huo, (Misitu, Idara ya Maji, RUBADA, RBMSIIP, NGO, n.k.), na pia utafitia emekuwa ukitekelezwa kwa miaka mingi.

9. **Baraza la Mazingira la Taifa lina dhamana kubwa sana kitaifa. Baadhi ya maeneo yanatia wasiwasi.**

**i) Je, kwa jinsi gani chombo hiki kinaweza kutoa maamuzi ya mwisho na serikali kuweza kuzingatia uamuzi huo, mfano, Mradi wa kamba inasemekana bado upo ingawa Baraza la Mazingira liliukataa huu mradi.**

ii) **Kumpa mwekezaji dhamana ya kutathmini athari za mazingira. Inahitaji kurekebishwa, mwekezaji asipewe nafasi ya kutathmini.**

- Kazi ya Baraza la Mazingira (NEMC) ni chombo cha ushauri na wala NEMC haina sheria. Inapotoa ushauri serikali inauwezo wa kuukataa au kuukubali.

- NEMC hutoa mwongozo/dodoso kwa mwekezaji jinsi ya kufanya tathmini na hatimaye NEMC kupitia tathmini hiyo. NEMC kwa kuzingatia maswala ya kimazingira inaweza kuukataa mradi au kuupitisha.

**10. NEMC ina majukumu makubwa lakini chombo chenyewe kinaning'inia. Kwa nini hakina sheria? Pia hakina mtiririko mzuri kama vyombo vingine vya serikali-Kuanzia ngazi za kijiji, wilaya mpaka Taifa.**

- Kazi ya Baraza la Mazingira ni kutoa ushauri kwa vitengo vinavyohusika (misitu, ardhi, wanyapori ndivyo vinavyochukua hatua za kisheria.

- Sasa hivi tuna rasimu ya kuanzisha kamati za mazingira. Inasubiri baraka za bunge. Hata hivyo sasa hivi kuna kamati za mazingira kuanzia ngazi ya kijiji, wilaya, mkoa hadi Taifa.

**11. Je, kuchimbwa kisima chenye uwezo wa kutoa zaidi ya lita 22,7000 kwa siku ni nani anayetoa kibali/hati?**

- Afisa maji wa wilaya ana uwezo wa kutoa hati ya kumiliki maji.

12. **Je, kijiji ambacho hakijasajiliwa wanaweza kuwa na milki ya ardhi?**

    - Si lazima kijiji kisajiliwe ili kumiliki ardhi. Kitu cha muhimu ni kama kijiji hicho kipo pale na kinatambuliwa na tawala zinazojulikana au kipo pale zaidi ya miaka 12.

13. **Je, Utatanishi wa mipaka kati aya kijiji na kijiji utafanywaje? Kuna vijiji ambavyo vina ugomvi wa mipaka yake**.

    - Upatanishi utapatikana kwa urahisi kwa kuweka majadiliano na kuwa na mipango ya pamoja ya kutumia maliasili zilizoko mpakani.
    - Ikishindikana mahakama inaweza kuchukua nafasi yake.

14. **Wakulima wa Bonde la mto Rufiji wanaogopa kulima mazao ya kudumu kwa kuwa wanasikia kwamba bonde lote linamilikiwa na Rais. Je, wananchi wanaweza kumiliki hilo bonde?**

    - Ardhi yote hapa nchini, Rais ni mdhamini na wala hamiliki ardhi.
    - Maeneo yote ndani ya **mita 60 kando kando mwa mito**, bahari, maeneo chepechepe ni maeneo yalitohifadhiwa (maeneo Mahasibu)
    - Milki katika maeneo mahasibu hayatolewi hati miliki.

15. Inasemekana ardhi yote iko chini ya Rais. Wakati huohuo maendeleo yote yanategemea ardhi. Iwapo ardhi siimiliki inamilikiwa na Rais, je, mwananchi inamsaidia vipi hii ardhi ambayo si mali yake?

    - Ardhi yote ni mali ya Umma, Rais ni mdhamini tu.
    - Hii haina maana kwamba watu hawaruhusiwi au wamezuiwa kuitumia. Mwananchi ni mmiliki hivyo ana uhuru wa kuiendeleza kama inavyostahili.

## 3.3 Majadiliano ya Vikundi Kuhusu Sera na Sheria

### 3.3.1 Kazi za Kufanya Katika Vikundi (Group discussion guidelines)

1. Eleza mambo yanayo kwaza/athiri utekelezaji wa sera na sheria ya mazingira mahali ulikotoka
2. Pendekeza mikakati inayoweza kutatua mambo au vikwazo vinavyo athiri utekelezaji wa sera na sheria ulizokwisha elelzea

### 3.3.2 Mgawanyiko Katika Vikundi

1. Sera na sheria za maliasili (misitu, nyuki, wanyama pori, na uvuvi)
2. Sera na sheria za mazingira, maeneo chepechepe, na maeneo yenye maji
3. Sera na sheria ya ardhi na kilimo

Vikundi vyote vitatu viliwasilisha ripoti zao na kuzielezea mbele ya wanasemina. Pale ambapo kulikuwa na upungufu, wanasemina waliongezea kile walichoona kinafaa. Wanasemina walionyesha umahili wao pale ambapo hawakuikubali taarifa ya kikundi cha tatu kilichojadili mada ya "sera na sheria ya ardhi". Kundi hili halikuonyesha bayana mikakati ya kuondoa athari zilizopo kwenye sera na sheria husika. Hivyo mwenyekiti wa semina ilibidi awape muda wa ziada wa kwenda kujipanga upya, kujadili na

kuwasilisha taarifa yao baada ya dakika 30. Walifanya hivyo hatimaye wanasemina waliipokea na kuikubali.

### 3.3.3 Majadiliano –Kikundi No. I

3.3.3.1 Mada: Athari za Utekelezaji wa Sera na Sheria za Mazingera (i.e. misitu, nyuki, uvuvi na wanyamapori)

**Athari**

1) Ushirikishwaji wa Maandalizi ya sera na sheria ni duni. Maandalizi hufanywa na viongozi wachache mfano: Viongozi wa ngazi za juu.
2) Wananchi wengi hawazifahamu sera na sheria kutokana na ufinyu wa elimu na upatikanaji wa taarifa
3) Umasikini unachangia utekelezaji wa sera na sheria kama uwekezaji
4) Kutoelewa kwa kina faida za maliasili zao
5) Tatizo la mipaka vijijini, Husabisha migongano
6) Wananchi kutofaidika na raslimali zinazovunwa kwenye maeneo yao, mfano, meli za uvuvi, ukataji ovyo wa mikoko, n.k.
7) Taratibu za utoaji vibali vya kuvuna miti

**Mikakati**

1) Jamii ishirikishwe katika kuandaa SERA na SHERIA.
2) Wataalam wapelekwe kwenye maeneo muhimu ya kazi
3) Wanachi waelimishwe kuhusu sera na sheria kwa kupitia redio, magezeti au mikutano.
4) Kuwepo na mipango ya kuinua kipato au uchumi wa wananchi wa vijijini ili kuondoa umaskini, mfano: Viandaliwe vikundi vidogo vidogo vya ushirika; Kubuni maeneo ya uwindaji ya vijijji, misitu ya vijiji, ufugaji wa wanyamapori, mifugo na kuboresha zao la korosho; Uundaji wa vikundi vya ufugaji nyuki, uvunaji asali kwa kuzishirikisha jinsia zote; na Ushirikishwaji wa wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori (KAMATI ZA MAZINGIRA ZA VIJIJI).
5) Wataalam wapelekwe kwenye maeneo muhimu ya kazi.
6) Serikali ipitie upya kwa uangalifu kupima, mipaka kijiji hadi kijiji, wilaya hadi wilaya , nchi kavu na bahari.
7) Kuwepo na udhibiti wa vyombo vya uvuvi
8) Serikali za vijiji zipewe uwezo wa kutoa LESENI katika uvunaji wa miti na samaki katika maeneo yanayohusika.
9) Fomu za maombi zijazwe (fomu ziko vijijini)
10) Fomu hizi zinaelezea wapi miti inatakiwa kuvunwa
11) Mvunaji aende kwanza anakotaka kuvunwa miti
12) Fomu inaletwa ofisi ya misitu, mtaalam anaandamana na mvunaji kwenda kuangalia miti anayotaka kuvuna. Endapo hakuna matatizo ya uharibifu wa mazingira, mvunaji anaruhusiwa kuvuna baada ya kutoa USHURU/ADA.

### 3.3.4 Majadiliano Ya Kikundi No. 2

3.3.4.1 Mada: Sera na sheria za Mazingira Maeneo Chepechepe na Maeneo Yenye Maji.

**Athari**

1) Ukataji miti ovyo, uchomaji moto ovyo misitu.
2) Uvuvi wa samaki wadogowadogo
3) Wanyama waharibifu
4) Utaalam duni katika kilimo cha kisasa
5) Kilimo cha kuhamahama
6) Ukosefu wa zana bora za kilimo (kwa mfano mashine za umwagiliaji maji)

**Mikakati**

1) Sera ndogondogo zitumike
2) Ushirikishwaji wa wananchi ufanywe kwa kuwaelimisha mambo yanayoathiri mazingira
3) Upandaji miti kuhifadhi maeneo chepechepe
4) Uvunaji wa miti midogo midogo ni marufuku
5) Uvunaji kwa kutumia misumeno ya mkono uzuiliwe
6) Vibali vyote vya uvunaji misitu vitolewe kwa kupitia serikali ya vijiji
7) Uvunaji uwe wa miti mikubwa tu
8) Uvunaji wa aina ya miti inayotishia kutoweka upigwe marufuku
9) Mipango ya uvunaji iwepo kwenye maeneo ya mradi
10) Nyavu za macho madogo chini ya inchi $2^1/_2$ zisitumike kabisa
11) Zana zinazotumia nyuzi za “monofilament” zinazotumiwa na meli kubwa zidhibitiwe
12) Kilimo cha bega kwa bega kiimarishwe ili kukabiliana na wanyama
13) Wananchi wahamasishwe katika kilimo cha kisasa pamoja na matumizi ya pembejeo.
14) Wananchi waelimishwe kilimo cha mseto na kubadilisha mazao.
15) Wananchi washauriwe kujiunga kwenye vikundi na kupatiwa misaada au mikopo.

### 3.3.5 Majadiliano ya Kundi Na. 3

3.3.5.1 Mada: Sera na Sheria za Kilimo na Ardhi

**Athari**

1) Sera na Sheria hazijawafikia washika dau
2) Migogoro ya mipaka
3) Uhaba wa wataalamu
4) Ukosefu wa mitaji
5) Matatizo ya matumizi ya ardhi
6) Kukosa masoko ya mazao/mifugo
7) Ukosefu wa Pembejeo
8) Rushwa
9) Mabadiliko ya hali ya hjewa
10) Wanyama waharibifu

**Mikakati**

1) Vifanyike vikao na mikutano ya sera na sheria
2) Sera na sheria vitolewe kwenye vyombo vya habari mfano magazeti na redio
3) Watu wa ardhi wapitie mipaka
4) Kukutana na wahusika ili wapatane
5) Kuandaa matumizi ya pamoja ya rasilimali zote zinazohusika na mgogoro
6) Wilaya iunde kamati maalumu za kusuluhisha mipaka
7) Wapatikane wataalamu wa kutosha na wasambazwe katika maeneo husika.
8) Wakulima wapate utaalamu wa ndani na nje ya nchi
9) Kushawishi vyombo vya fedha vitoe mikopo ya riba nafuu
10) Kuanzisha vikundi vya ushirika ili iwe rahisi kupata mikopo
11) Vijiji viandae matumizi bora ya ardhi
12) Elimu itolewe juu ya matumizi bora ya ardhi
13) Tuimarishe Vyama vya ushirika
14) Tuwakaribishe wawekezaji/wafanya biashara
15) Tuimarishe vyama vya ushirika
16) Tuimarishe ufugaji ili tupate mbolea ya samadi
17) Tupokee taarifa za wataalamu wa hali ya hewa, mfano kwa kupitia redio au magazeti na kuzifanyia kazi
18) Kulima kwa pamoja ili kuzuia kwa pamoja
19) Kuunda vikundi vya usakaji wa wanyama waharibifu
20) Wanyama wakali wadhibitiwe
21) Kutopokea wala kutoa rushwa

# 4 Mada zilizoongelewa (Mei 5, 2000)

## 4.1 Hali ya sasa ya Uangushaji Na Uvunaji Misitu Wilayani Rufiji

(Ndugu Abdalla Shah, Meneja wa MUMARU)

Utafiti kujua kiwango cha uvunaji miti ulifanywa mwezi we Februari 2000 kwa kutumia ndege eneo lililo kati ya UTM 420000 na UTM 520000. Utafiti umeonyesha kulikuwa na visiki vipya 11,000 na vya zamani 74,000 katika wilaya nzima ya Rufiji. Hesabu za haraka haraka mti mmoja (1) unatoa mbao 12 na kila ubao 1 unauzwa Tshs. 2,000 (Hapa Rufiji) na Tsh. 10,000 (Bei ya Dar es Salaam).

**Thamani ya miti 11,000 kwa mwaka**

Wilayani Rufiji: Miti 11,000 x mbao 12 x Bei Sh. 2,000.00 = 264,000,000.00
Dar es Salaam: Miti 11,000 x mbao 12 x Bei Sh. 10,000 = 1,320,000,000.00

- Mahesabu haya yanaonyesha kwamba kasi ya uvunaji miti wilayani Rufiji ni kubwa sana na baadhi ya miti imeanza kuwa adimu (mivule, mininga na mipingo). Mikongo nayo inaanza kuwa adimu.
- Makisio haya ni ya chini sana lakini yanaonyesha mapato makubwa. Changamoto kwa wanasemina –kujadili jinsi ya manufaa yatakavyorudi hapa Rufiji.
- Msitu wa Weme mashariki unahitaji ulinzi mkubwa. Usipovunwa kwa sasa, hapo baadaye miti hii itakuwa na thamani kubwa zaidi.
- Wa-rufiji wanapata faida ndogo zaidi ikilinganishwa na wanayopata wafanya biashara ya mbao na magogo.

## 4.2 Rasilimali ya Miti ya Mbao Katika Wilaya ya Rufiji

(Ndugu Stephano- Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine - Morogoro)

Ulifanywa utafiti wa miti ya mbao kukadiria idadi na majina au aina ya miti. Misitu mitano ilitembelewa (1) Mbunju Mvuleni (2) Mtanza Msona (3)Utete (4)Weme (5)Kichi. Kuna aina ya miti 247 na aina 24 zinafaa kwa upasuaji mbao. Miti aina ya Mfuru, Mtanga, Mkwaju, Mlondondo, Mag'ongo, Mnyegea, Mkwara, Mseru, Msolo, Mgude, Mvumo, Mnee na Mbugubugu inafaa kwa mbao lakini wananchi hawaipendelei. Watafiti wanashauri matumizi ya hii miti na kuacha kuvuna miti inayotaka kutoweka aidha kwa ajili ya kuwa na uoto hafifu au inavunwa kwa kasi. Miti inayovunwa kwa kasi ni Mkongo, mpingo, mninga, mvule, mmangu na msenga. Misitu ya Mtanza Msona imevunwa kwa kiwango cha hali ya juu kuliko maeneo yote yaliyokwisha fanyiwa utafiti.

## 4.3 Uhifadhi wa Mimea Mbalimbali Katika Wilaya ya Rufiji

(Ndugu L. Mwasumbi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

Utafiti ulifanywa kwenye misitu ya Ilu, Weme na Kichi. Ilu kuna aina za mimea 90, Weme 144 na Kichi aina 143.

- Misitu ya mlima wa Kichi inafaa kuhifadhiwa na kufanya shughuli za utalii (Ecotourism); kwa ajili ya elimu, hifadhi mazingira.
- Kuna aina mbili za mimea ambayo ina nguvu ya madawa *Cleistoclamys Kirkii, Polyalthia tanganyikensis*.

## 4.4 Uhifadhi wa Wanyama wa Aina Mbalimbali

(Ndugu Kihaule, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni Weme na Kichi. Unaweza kutambua kuwepo kwa wanyama wa aina fulani kwa kutumia (1) Mitego (2) Sauti (3) Wenyeji (4) Alama mbalimbali –(Kinyesi, alama za kwato

n.k). Kichi na Weme kuna Wanyama wanyonyeshao aina 30, Vyura n.k. aina 32. Mijusi na Nyoka aina 16. Utafiti huu unaonyesha kwamba wanyama wadogo wadogo ni wachache sana.

1. **Mchango/majadiliano (siku ya tatu ya semina)**

**Kuna aina ngeni ya wanyama wadogowadogo inayopatikana hapa Rufiji**

- Aina Fulani ya vyura, nyoka.

2. **Dawa za kukaushia wanyama zinaitwaje**

- Formalin

3. **Je, hawa wanyama wadogowadogo wapo ambao wanaweza kutumiwa kama dawa?**

- Hakuna.

4. **Je, hizo voucher Specimen zinaweza kuletwa hapa Rufiji ili nasi tuwe na kumbukumbu hizo**

- Mkihitaji mtaletewa, lakini kuna jinsi ya kuzihifadhi. Maandalizi thabiti yanahitajika kama makabati ya kuhifadhia.

5. **Je, kwa nini mikoko haikufanyiwa utafiti kujua kiwango kinachovunwa kwa kutumia ndege.**

- Miti ya mikoko ina unene mdogo ambao visiki nyake haviwezi kuonekana kwa kutumia picha za ndege. Hata hivyo kuna njia zingine za kuhesabu uvunaji mikoko kama kuangalia maeneo yaliyokatwa mikoko na kubadilishwa kwa mashamba ya mazao ya chakula.

6. **Uvunaji misitu usimamishwe kwa muda. Wakati huo huo njia zingine za kukidhi maisha zitafutwe. Mfano, kuwapa mitaji wale wanaotegemea shughuli za misitu ili waanzishe shughuli zingine ndogondogo kama ufugaji nyuki, kilimo na uvuvi.**

- Kufunga uvunaji miti siyo ufumbuzi wa tatizo la kutoweka misitu yetu. Ikumbukwe kwamba Halmashauri ya Wilaya inategemea sana misitu katika kuendesha shughuli zake za maendeleo. Ningeshauri tuunde bodi za wadhamini za kudhibiti mapato na matumizi yatokanayo na misitu na maliasili zingine.

## 4.5 Maoni ya Wanasemina

1) Vibali/ruhusa inatolewa na wataalam. Wakulima/wananchi inakuwa vigumu kuzuia kisheria.
2) Taarifa zote zilizotolewa na wataalam/watafiti ni lazima zifanyiwe kazi.
3) Wanatoa vibali vya kukata miti ni lazima wazingatie taratibu
4) Msitu wa Weme mashariki unahitaji ulinzi mkubwa sana. Usipovunwa leo, hapo badaye miti hii itakuwa na thamani kubwa sana.
5) Tumesikitishwa sana na kasi ya uvunaji wa misitu yetu. Idadi ya miti inayovunwa tuliyopewa ni ndogo sana ukilinganisha na hali halisi. Utafiti kama huu ufanyike kila baada ya mwaka mmoja ili kuelewa mwenendo wa uvunaji miti. Pia tunasikitika sana kuendelea kuwa masikini wakati tuna utajiri wa maliasili, wakati huohuo maliasili za Wa-Rufiji zinawatajirisha watu wa nje.

# 5 Maoni ya Jumla

1) Wanasemina wameahidi kuwa waalimu wa watu ambao hawakuwepo kwenye semina.
2) Watu wapande miti kwanza ndipo wakate mti
3) Ifanywe semina inayowahusisha viongozi wengi wa vijiji
4) Vikao kama hivi vifanyike mara kwa mara
5) Wataalam watimize wajibu wao wakishindwa wawaachie wenginewenye uwezo.
6) Wataalamu wafike vijijini kutoa semina mbalimbali
7) Utaalamu uhamishishwe toka maofisini au sehemu uliko kwenda sehemu nyingine
8) Watu waelimishwe uwiano kuhusu umilikaji wa ardhi bila kujali jinsia
9) Wananchi wapo tayari kupanda mikoko hivyo mipango ifanywe mapema kabla ya mwezi wa saba

9. Utafiti wa zao la samaki aina ya kamba ufanyike ili kujua wapo kamba kiasi gani
10. Maeneo ya uvuvi wa meli kubwa yabainishwe ili kujua umbali gani wanaoruhusiwa kuvua toka ufukweni au kwenye midomo ya mito ili kuondoa kero ya uharibifu wa mazalio ya samaki vile vile kero ya uharibifu wa zana za wavuvi wadogowadogo.
11. Yatengwe maeneo maalumu kwenye bahari ambapo wavuvi wadogowadogo watakuwa wanafanyia shughuli zao. Maeneo haya yawe ukanda mzima wa ufukwe wa bahari.

10) Mipango bayana ya uvuvi iandaliwe katika vijiji vya mradi.

# 6 Kufunga Semina

Semina ilifungwa rasmi saa 8.40 mchana. Semina hii ilifungwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Rufiji kwa niaba ya mkuu wa wilaya. Aliwakumbusha wana semina kuwa wao ni wawakilishi wa wenzao walioko majumbani. Yale yote waliyoyapata katika semina hii wayapeleke kwa watu katika maeneo yao ili yafanyiwe kazi. Wilaya ya Rufiji ina maliasili nyingi, lakini watu wake bado wanaendelea kuwa maskini na mazingira yao yanaharibika. Kwa kuyatekeleza yale yote tuliyoyapata kwenye semina hii. Nina imani umasikini na uharibifu wa mazingira vitapungua kama sio kutoweka kabisa.

Katika semina hii tumeona kwamba Baraza la Kuhifadhi Mazingira (NEMC) halina sheria. Tunaomba sheria zitungwe ili Baraza hili liwe na nguvu kisheria.

Kwa hayo mafupi nina tamka rasmi kwamba semina hii imefungwa.

## 6.1 Hotuba ya Kufunga Warsha

Iliyotelewa na Ndugu F. Q.M. Fissoo – District Executive Officer

Mh. Mwenyekiti wa Halmashauri, Mh. Makamu wa Mwenyekiti, Wahe. Madiwani, Wataalam mbalimbali na washauri wa Mradi, Wanavijiji, Wahamasishaji wa warsha.

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa uongozi wa MUMARU (REMP) kwa kuandaa warsha hii ya siku tatu iliyojadili sera na sheria zinazohusu mazingira na hali halisi ya maliasili ya wilaya ya Rufiji. Waheshimiwa Madiwani, wanavijiji na wataalamu wamepata heshima kubwa sana na utaalamu kutokana na warsha hii ya mazingira. Wamepata heshima kutokana na ushiriki wa hali ya juu uliojumuishwa katika ratiba ya Warsha hii. Taarifa nilizopata ni kwamba washiriki wote wameshiriki kikamilifu kuanzia mwanzo wa warsha hadi wakati huu ninapofunga warsha. Hii ni dalili ya wazi kwamba wanawarsha wako tayari katika kusaidia suala la Hifadhi ya mazingira.

Wataalamu kutoka sehemu mbalimbali walishiriki kwenye warsha hii, Baraza la Taifa la Hifadhi ya mazingira (NEMC), Tume ya Ardhi na Mipango, Wizara ya Maliasili na Utalii, Vyuo vikuu vya SUA na UDM. Hao wameweza kutoa ushauri wa kitaalam kwa kutumia majadiliano na wanawarsha na viongozi wa ngazi nilizozitaja hapo juu wilayani pamoja na wataalam wa idara za halmashauri.

Wilaya ya Rufiji ina maliasili na raslimali nyingi: Ardhi, misitu, samaki, wanyamapori, nyuki n.k. lakini wananchi bado wanakabiliwa na tatizo la umaskini na matumizi mabaya ya rasilimali hizo.

Tunashindwa kuelewa kwamba ardhi, wanyama na viumbe hutegemeana na sisi tunategemea vyote hivyo, na kwa sababu hiyo ni lazima tuvitunze. Tunashindwa kuelewa kwamba kila tunapoharibu misitu kwa uchomaji moto au kwa uvunaji wa ovyo ovyo, tunaharibu maeneo chepechepe ambayo ni vianzio vya maji, tunaharibu biomiwai na hivyo uoto wa viumbe hai. Matokeo ya uharibifu wa mazingira ni kukosekana kwa mvua, ukaukaji wa mito na mmomonyoko wa ardhi. Hatima yake ni kuongezeka kwa umaskini na vifo vya viumbe hai.

Katika warsha hii, tumejulishwa kwamba zipo sera na sheria mbalimbali kuhusu mazingira, kama vile sera ya misitu, nyuki, uvuvi, wanyamapori, mifugo, kilimo, ardhi n.k. pamoja na sheria zake. Pia tumejulishwa kuhusu vyombo mbalimbali vya kiserikali na visivyo vya kiserikali vinavyosimamia mazingira. Vyombo hivyo vinatakiwa kufanya kazi kwa mahusiano na kutegemeana.

Mkusanyiko huu ulikuwa na kazi kubwa ya siku tatu ya kutoa ufafanuzi, kujadili na kuchambua sera na sheria za mazingira na ardhi. Watoa mada na washiriki wa semina mmeonyesha kuiva katika uwanja wa Hifadhi Mazingira kwani siku zote hizo muliweza kuzichambua hizo sera kwa undani na hatimaye kufikia maoni au mawazo ambayo hapo baadaye mradi wa mazingira “MUMARU”, Serikali na wananchi wote wa Rufiji watayafanyia kazi. Kero kubwa kwa wilaya yetu ni uharibifu wa mazingira na umasikini uliokithiri. Nina imani kama yale yote mliyoyaongelea katika semina hii yatatekelezwa ipasavyo, uharibifu wa mazingira utapungua na umasikini pia utapungua kama sio kutoweka kabisa.

Wanasemina ni wawakilishi wa wananchi, hivyo ni lazima yale mliyoyapata hapa tuwafikishie wale tuliowawakilisha. Kwa ufupi tukawaeleze wananchi kwamba ni lazima tuwe na mipango madhubuti ya maendeleo kwa kutumia kwa uangalifu mali asili tulizonazo, yaani tuwe na matumizi endelevu. Kila mmoja wetu ni mtekelezaji wa hizi sera ili hatimaye tufikie malengo tuliyojiwekea.

Kuna mapendekezo yaliyotolewa katika warsha hii. Moja ya mapendekezo hayo ni kwamba itungwe sheria ya mazingira itakayoipa NEMC uwezo wa kisheria wa kushirikisha sekta zote, uwezo wa kisheria wa kusimamia utekelezaji wa sheria na utendaji katika masula ya hifadhi ya mazingira. Pamoja na mapendekezo hayo, nami napendekeza kwamba mfumo wa kusimamia na kuhifadhi mazingira uwajibishe ngazi zote kuanzia kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa adi Serikali Kuu. Elimu ya mazingira ifundishwe katika shule za msingi, vyuo na taasisi zote za elimu.

Baada ya Warsha hii, ni imani yangu kwamba wananchi wote wataelimishwa na kuhamasishwa katika masuala yote ya kusimamia na kuhifadhi mazingira. Baada ya maelezo haya mafupi, natamka rasmi kuwa Semina yenu imefungwa rasmi na ninawatakia safari njema.

*Asanteni.*

# 7 Appendices